

KUSHAWISHIKA KISHA KUHUSIKA



Asante, sana, Ndugu Parker.

Habari za jioni, marafiki. Ni vema kuwa hapa usiku wa leo tena. Nami nadhani mmechoshwa na kuketi, kunisikiliza mimi. Nami nili—nilichoka sana, nikapwelewa na sauti, kidogo nimepwelewa na sauti kutokana na kuhubiri kwa nguvu sana.

² Nilikuwa tu nikizungumza na Ndugu Parker pale, na kumwambia ya kwamba ninaamini huu ndio mmoja wa mikutano mizuri kuliko yote ambayo Bwana ameturuhusu kuwamo katika muda mrefu. Haijakuwa mikubwa, mnajua ninalomaanisha, bali si mikubwa kupita kiasi. Hapajakuwapo na wengi mno wanaoihudhuria, lakini u—u—ubora wake, umekuwa wa ajabu. Imani, jamani, inaonekana kana kwamba chochote kingeweza kutokea. Ninapenda mkutano wa namna hiyo ambapo unajisikia tu kama kwamba chochote chaweza kutokea wakati wowote. Na mimi—mimi napenda hilo. Nami nina hakika kutakuwako na matokeo ya kudumu, nayo yatajionyesha.

³ Hakika ninavutiwa na subira yenu nyote, kuketi, mkinisikiliza nikihubiri kwa saa kadhaa, kisha mnarudi usiku unaofuata. Kweli mnaweza kustahimili adhabu nyingi sana. Mnaona? Kwa hiyo mimi... Ninajua mna subira nyingi sana nzuri. Kwa hiyo sisi...

⁴ Ninataka kusema, kwa ajili yetu sote, kwamba tunawashukuru, yule Ndugu Thomas. Siwezi kabisa kuelezea hisia zangu kwa ajili ya Ndugu Thomas. Yeye, nilidhani nilimfahamu, bali nilikuwa nimemfananisha na mtu mwingine. Nilipata kusalimiana kwa mikono na maskini mke wake, wa thamani. Nao kweli ni watumishi wa Kristo. Nami bila shaka ninatumaini kwamba, Mungu akipenda, kwamba njia zetu zitakutana, mara nyingi zaidi, maishani.

⁵ Kama ningalikuwa ninyi watu, nami niliishi karibu na hapa, kanisa lake lingekuwa ndipo mahali ningekuwa nikihudhuria. Kwa hiyo na—nawapenda, mtu ambaye...

⁶ [Ndugu Parker Thomas anasema, “Nachukia kumkatiza Ndugu Branham namna hii, bali nafikiri itakuwa ni sawa kwenye wakati huu. Namshukuru kwa hizo sifa na mambo hayo mazuri aliyosema. Sijui tu kama watu walio karibu na hapa, na wote wanaohudhuria mkutano huu mkubwa, wangemtaka arudi tena. Vipi kuhusu hilo? Kila mtu anataka hilo?” Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. [“Kwa kweli, mngemtaka aje Juni ijayo na—na kuketi tu pamoja nasi? Kama mnataka, simameni kwa miguu yenu. Hima.”] Asanteni. [“Vema. Ketini.”]

⁷ Asanteni, sana. Hilo ni zuri kweli. Asante, Ndugu Parker. Ninaninii sana...[Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]

⁸ Alisema matumizi yote yamelipiwa, na kila kitu. Tunathamini ushirikiano mzuri wenu nyote, usaidizi, maana, mwajua, ina gharama kufanya mikutano hii mikubwa. Na kwa hiyo kila kitu kimelipiwa. Hilo ni jema kabisa. Tunashukuru tu. Kila kitu, hakuna deni.

⁹ Bwana ameokoa, ameponya, na kila kitu kimetukia, kwa hiyo tuna furaha tu kuwa vile...kuona jambo hili. Nachukia kuona mkutano huu ukiingia katika historia. Lakini utakuja tena kwenye...Huko nyuma kabisa, katika nyakati zijazo, tutaona matokeo.

¹⁰ Sasa tunataka kumshukuru kila mtu tena kwa, nataka kuwashukuru, kwa ajili ya maskini zawadi ambazo mlinitumia kwenye wakati huu. Ninathamini hilo sana, sana.

¹¹ Na sasa, tunaenda huko chini sasa kumtembelea Ndugu Bigbee huko Carolina ya Kusini, Columbia, Columbus, Carolina ya Kusini. Na sisi tunapaswa kuwa huko kesho usiku na Jumanne usiku, pamoja na Ndugu Bigbee. Kisha tutaelekea kwenye Pwani ya Magharibi.

¹² Ninataka kuwaulizeni, halafu basi, kutoka huko, nadhani, tukiisha kuumaliza uamsho huu huko juu, ninataka kwenda Afrika, Australia, New Zealand, na kupitia kule. Ninaweza kuyategemea maombi yenu kwa ajili yangu, kwamba Mungu atanisaidia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi asanteni sana.

¹³ Nasi tunashukuru sana kwa ajili ya mambo yote. Ninasema hilo kwa ajili yangu mwenyewe na kwa ajili ya watu walio hapa kutoka kwenye maskani. Nina nanii wetu...ama baadhi ya wadhamini wetu hapa, na mashemasi, na baadhi ya marafiki zangu kutoka kule chini.

¹⁴ Mchungaji wetu yupo hapa. Kamwe sijaweza kumwona Ndugu Neville. Nadhani ametambulishwa. Sivyo? [Ndugu Parker anasema, "Naam."—Mh.] Naam. Ndugu Neville. Uko wapi, Ndugu Orman. Kamwe siwezi kukutambua. Na, loo, jamani! Kule nyuma, mkubwa tu vile vile. Njoo hapa kwa dakika moja.

¹⁵ Mtu huyu, ninamjua kuwa ni mtumishi wa kweli wa Kristo. Alikuwa Mmethodisti mgumu kwelikweli, kisha akampokea Roho Mtakatifu. Sasa yeye ni Mmethodisti wa Roho Mtakatifu. Huyu ndiye mchungaji wetu wa thamani.

¹⁶ Ninataka kukupa mkono, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Asante. Mungu akubariki. Vema kukuona."—Mh.] Asante. Mnavyo viti... .

¹⁷ Nimemfahamu Ndugu Neville kwa miaka kadhaa, na maskini mke wake, mpendwa, hata kabla hawajafunga ndoa. Nayo miaka ambayo nimemfahamu, yeye hajabadilika hata kidogo, ni kwamba tu alipanda juu zaidi katika Mungu. Hivyo tu. Lakini anaweza kutegemewa. Tunampenda sasa kama mchungaji. Amekuwa hapo ndani kwa miaka kadhaa, nasi tunatumaini atakaa mpaka Yesu atakapokuja, yakiwa ni mapenzi ya Bwana.

¹⁸ Basi ungetaka tu kusema neno kwa hawa watu, Ndugu Neville?

¹⁹ [Ndugu Neville anasema, “Vema, nina furaha sana kuwa hapa pamoja na mtu huyu mwema wa Mungu, ambayo yamekuwa ni majaliwa yangu kushirikiana naye miaka hii kumi. Sijui kama nimekuwa Gehazi mzuri, ama la, lakini nimejaribu kumbebea fimbo huyu mtu wa Mungu. Yeye ni zaidi ya rafiki kwangu. Amekuwa, tuseme, baba katika Injili, kwangu mimi, pia, ingawa nimempita kwa miaka michache katika umri—Mh.]

²⁰ [“Lakini, hata hivyo, nimefurahi sana, pia, kuwa kwenye mkutano huu. Kitu fulani kilinishika hapa chini katika Southern Pines, kwamba napenda mahali hapa vizuri sana. Nami nimepafurahia mno. Ninajua kwamba Mungu alihusika katika mimi kuweza kuja hapa na kuwa pamoja na Ndugu Branham katika mkutano huu. Kwa hiyo, nimefurahia sana kuwa hapa, kwamba mambo yamekuwa shwari na ya ajabu sana, hata siwezi kumsifu Bwana vya kutosha, usiku wa leo, kwa ajili ya haya yote.]

²¹ [“Lakini, zaidi ya yote, nilisema, nilipokuja hapa, lipo jambo moja linaloangaza mkutano wote kwangu mimi, na hilo ni Neno hili la Mungu. Amina. Nisingeninii. . . Nisipomwona mtu akiponywa, nisipomwona mtu yeyote akiwaombea wagonjwa, kama Mungu akiendelea tu kunipa mimi Neno Lake, hiyo hapo furaha inayojaza nafsi yangu, nayo hutoka chini ya miguu yangu hadi utosi wa kichwa changu, Neno hili la Bwana. Na, amina.]

²² [“Nimefurahia kwamba Mungu ameyabariki majira haya ya mtumishi na nabii wa Mungu. Nami nimeihisi Baraka ikitoka kwake ikaja kwangu, kwa hiyo nina furaha niliweza kufika hapa. Natumaini nyote mlihisi jambo lile lile nililohisi, katika ibada hizi. Mungu kweli amembariki mtumishi Wake huku chini mahali hapa. Sababu ya mimi kujua hivyo, yeye alilielezea hilo kitambo kidogo kilichopita. Na mambo makuu na yenye nguvu tuliyo nayo katika Imani, usiku wa leo!]

²³ [“Baba, Biblia inatufundisha, haitubidi kuwa na mambo yanayoonekana. Yote tunayohitaji ni kwamba, tuombapo, tuamini, nasi tayari tumeyapata. Amina. Ninayo sasa, kwa sababu hivyo ndivyo Biblia inavyosema yalivyo. Nami ninapendezwa sana na hilo, kwa sababu Mungu anafanya

mambo haya ya ajabu kupitia kwa huyu, mchungaji wetu, Mtumishi wa Mungu na nabii, Ndugu Branham. Bwana na ambariki daima na aendeleo kumweka katika Njia hii. Bwana asifiwe!”]

Mungu akubariki, Ndugu Neville, kutoka moyoni mwetu mwote.

²⁴ Sasa, mnajua, unapofanya mandari, kama mtu fulani alipigilia mti mdogo mahali fulani, vema, huwezi, hujui kama ungali pale ama haupo, unaona, maana umewekwa tu huko, ukapigiliwa huko, ama kitu fulani. Lakini unapojua kuna mwaloni wa kale ambao umekaa pale imara, unaweza kuwazia vizuri sana kuhusu kwenda chini ya mti huo na kupumzika. Huyu ni Ndugu Neville, vile vile tu kila siku, akisonga mbele tu moja kwa moja. Kwa hiyo nina furaha sana kwa hilo.

²⁵ Tunaye—tunaye ndugu mwingine hapa, maskini mchungaji, moja ya makanisa yetu dada kule chini. Kama haji huku, ningemtaka asimame, Ndugu Junior Jackson, Mmethodisti mwingine aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Junior Jackson, uko wapi? Ndugu Junior Jackson, Mmethodisti, aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Huyu hapa, papa *hapa*, Ndugu Jackson. Unataka kusema jambo fulani, ama lolote unalotaka kusema? Vema.

²⁶ Mwingine hapa ni Ndugu Palmer, mwingine wa ndugu zetu hapa. Waweza kusimama tu, Ndugu Palmer? Mchungaji kutoka huko chini Macon, Georgia, ni mmoja wa marafiki zetu.

²⁷ Na Ndugu Fred Sothmann, ninajua yupo hapa. Ni mmoja wa wadhamini wetu kanisani. Uko wapi, Fred? Mahali fulani hapa ndani, ameketi nyuma huko nyuma.

²⁸ Ndugu Banks Wood, uko wapi, Ndugu Banks? Yeye ni mmoja wa wadhamini wetu wale wengine, *hapa*.

²⁹ Ndugu Banks alikuwa ni Shahidi wa Yehova, mwajua. Ndipo akaja mkutanoni, naye alikuwa na mvulana kiwete, David, mguu wake umekunjamana, kutokana na polio. Nami nilikuwa kwenye mkutano wa hema, na kwanza alikuwa ameona ninii. . . . Alikuwa huko—huko Dallas, usiku huo. . . . ama, Houston, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka katika mfano wa ile Nuru, nao wakapiga picha Yake. Ndugu Wood alikuwa kule. Kwa hiyo, sikumjua wakati huo. Na kwa hiyo akakusanya fedha za kutosha. Yeye ni kondrakta. Akaja kwenye mkutano uliofuata. Mimi nikaenda nchi za ng'ambo, kutoka huko, kisha nikaenda kwenye mkutano wa pili. Alikuwa na mvulana wake kiwete, na polio. Basi wakati tulipokuwa. . . . Nilikuwa nimesimama pale chini ya upako wa Roho Mtakatifu, karudi kupitia huo umati, kazungumza naye. Kamwambia yote kuhusu hilo. Kamwambia asimame.

³⁰ David, uko wapi? Upo hapa, usiku wa leo? Naam. Yule mvulana aliyekuwa kiwete, huyo ndiye. David, endapo watu hawaamini kwamba Mungu anaweza kumponya mtu ambaye mguu wake umekunjamana kwa polio, na kadhalika, laiti

ungalitembea tu hapo nje, kwa dakika moja tu, uwaonyeshe jinsi unavyoweza kutembea. Naam. Naam. Hapa, sio tu kufanya maonyesho ya umma, bali ushuhuda tu. Hapo, mnaona, hamna hata kuchechemaa au chochote kile, mkamilifu na mzima kabisa. Mnaona? Ni ajabu kweli, kweli, yale Bwana wetu anayoweza kufanya. Sasa, kama Yeye atafanya hivyo kwa ajili yake, mbona, Yeye atalifanyia mtu mwingine. Mnaona? Kwa hiyo, hakika, ni kwamba tu kama tunaweza kupata imani ya namna hiyo.

³¹ Sasa, hakika, nyote mnamfahamu, kumjua Ndugu Ben hapa chini. Yeye alinirii tu...mwajua, mtu huyu mnayeweza kumsikia juu ya kila mtu, akisema, “Amina.” Nitawasimulia kidogo. Ninachukia kusema jambo hili juu yake; mke wake akiketi pale. Sote tunampenda Ben. Nayo ilikuwa ni kabla hajaoa. Nilikuwa kwenye Pwani ya Magharibi. Naye mvulana huyo ametoka Indiana kusini.

³² Nilikuwa huko nje kwenye Pwani ya Magharibi, nikihubiri tu, huko usiku mmoja, Bonde la San Fernando, bondeni, pamoja na Wabaptisti, hema kubwa lililojaa watu. Sasa, hao kwa namna fulani ni watu wangwana, mwajua. Nami nilikuwa nikiendelea tu kuhubiri. Moja kwa moja nikasikia kishindo; nywele nyeusi za matimutimu, zikitikisika, kama—kama—kama—kama Mmekisiko; miguu miwili mikubwa ikirushwa hewani; mikono yake namna *hiyo*. Nikasimama. Nikasema, “Ben, kwani ulifikaje huku nje kamwe?” Alikuwa ndiye huyo hapo.

³³ Mungu akubariki, Ben. Hutaafanya zaidi ya kusimama tu, simama tu, wewe na mke wako. Tungewataka tu watu waninii...Ndugu Ben, huyo ndiye amekuwa akisema hizo “amina” zote hapa chini kwenye kona *hii* hapa. Mungu awabariki. [Ndugu Ben Bryant anasema, “Natamani maombi yenu nyote. Tunatumaini kurudi kwenye huduma ya umishenari, kabla ya kitambo kirefu, huko milimani, Ndugu Branham.”—Mh.] Amina. Mungu awabariki.

³⁴ Ndugu Way, mmishenari mwingine, akijaribu kuingia katika huduma za kimishenari. Yeye yuko pamoja nasi, usiku wa leo. Tunamfahamu. Amekuwa akikaa kwetu kwa kitambo kidogo. Uko wapi, Ndugu Way? Uko mkutanoni? Papa *hapa*, pamoja na mke wake. Na sasa, nawaambia, vita kati ya Uingereza na Norwe vimetatuliwa. Yeye ni Mwingereza, naye mke ni Mnorwe. Vimekwisha. Watu wa kupendeza. Naam, bwana. Vita vimekwisha.

³⁵ Ndugu Boze alikuwa huku, hivi majuzi usiku, akionyesha picha yake, na kusema, “Loo, vema,” akasema, “yupo mwanamke...” Huyu ni Dada Sothmann. Na laiti ningalimfanya asimame, pamoja na Fred, hapa ndani mahali fulani. Watu wa kupendeza. Naye ni Mnorwe. Hakika, Ndugu Boze ni—ni Mswedi. Naye alisema, “Hum! Hum!” Mnajua vile Joseph afanyavyo. Kasema, “Yupo mama fulani hapa, dada

fulani,” kasema, “yeye ni Mnorwe.” Kasema, “Hakika, iwapo huwezi kuwa Mswedi, ni vema kuwa Mnorwe.”

³⁶ Tukatoka nje, akaniangalia. Ndipo nikasema, “Hakika, Joseph, ni vibaya sana kwamba wote hawawezi kuwa ni Airishi, Waairishi.” Kwa hiyo sote tuna ucheshi kule chini.

³⁷ Ndugu Higginbotham, uko wapi? Mahali fulani hapa, vema, mtu mwingine mtauwa kutoka kwetu. Mtu aliyekuwa mdhamini kanisani huko chini, kwa miaka na miaka. Na rafiki yake, Dada Arganbright, Dada Ruth Arganbright, papa hapa. Ninaamini yeye ameketi hapa nje kwenye marefu ya kanisa. Simama. Ni wangapi wanaomfahamu Minor Arganbright? Mmoja wa makamu wa rais wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, binamu yake.

³⁸ Loo, jamani! Nikimkosa yeyote wenu jamaa! Ni, ninawajivunia, kila mmoja. Nina furaha mko hapa pamoja nasi. Hatujui, tukiingia na kutoka.

³⁹ Ndugu na Dada Dauch wanaoketi pale, pia, na Dada Brown, Ndugu Brown.

⁴⁰ Ndugu McKinney, mhubiri mwingine Mmethodisti aliye na Roho Mtakatifu. Uko wapi, Ndugu McKinney? Uko wapi, karibu na hapa? Ametoka huko Ohio. *Hapa*, huku nyuma kabisa, mwingine mwenye ujuzi kamili, aliyezaliwa katika Neno hili, Mmethodisti aliyetikiswa akatoka. Hiyo ni kweli. Sasa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, akisonga mbele kwa ajili ya Mungu.

⁴¹ Pat Tyler, rafiki mwingine msiri wangu aliyeketi huku. Ndugu Pat, simama. Nyote huenda mnamfahamu Pat Tyler. Asante, Ndugu Pat. Mungu akubariki. Yeye alikuwa mhalifu, jambazi, mwuaji. Mungu alimwokoia na kumfanya mtakatifu. Anaomba lifti kote nchini, apate kuifuatilia mikutano na kadhalika.

⁴² Mnajua yale ninayowazia juu ya watu hawa, ambako wametoka? Ninawazia juu ya Waebrania, mlango wa 11, “Walikatwa kwa msumeno, wakazunguka-zunguka wakivaa ngozi za mbuzi na ngozi za kondoo, ambao ulimwengu haustahili kuwa nao.” Wote wanabeba ushuhuda wao.

⁴³ Tom Simpson, yuko wapi Tom? Je, alikuja? Nilidhani niliona gari lake hapa nje. Yeye na familia yake, nilidhani alikuwa hapa. Labda nilikosea. Naam. Kuruka-ruka juu chini kama kuuma ugwe wa kuvulia huko nje, “bump-bump,” namna hiyo. Vema.

⁴⁴ Bwana awabariki ninyi nyote. Tuna furaha kuwa hapa. Hawa hapa wengine kutoka Georgia, mahali mbalimbali. Na sisi tuna furaha ninyi nyote mpo hapa, na kukutana, na marafiki zetu wa siku nyingi.

⁴⁵ Hivi ninamwona Dada Peckinpugh kutoka Chicago? Nilidhani nilikuwa. Na Dada Little, na huyo aliye karibu naye, na—na Dada D’Amico, watu wa thamani, wapendwa kutoka

Chicago, kundi hilo la wanawake ambao wamekuwa wapendwa sana kwangu.

⁴⁶ Na wengine wanaoketi hapa. Ndugu, hata siwezi kulikumbuka jina lake, na kutoka huko chini Georgia mahali fulani. Mimi... Yote hayo, loo, jamani, ni kama wote wameshikamana huku. Tuna furaha kuwa katika ushirika huu.

⁴⁷ Mzee Ndugu Bosworth alizoea kuniambia, akasema, “Ndugu Branham, unajua ushirika ni nini?”

Nikasema, “Nafikiri ninajua.”

⁴⁸ Akasema, “Ni jamaa wawili kwenye meli moja tu.” Kwa hiyo haya basi, bali tuna ushirika. Bwana na awarehemu.

⁴⁹ Asanteni kwa yale yote mliyofanya. Na mimi nitaandika mmoja wa hii, mkutano huu, katika orodha yangu, kama mmoja wa kumbukumbu muhimu za siku zangu za huduma, kwa ajili ya ushirikiano wenu mzuri, ndugu hawa wazuri na dada, na kila mtu ni mkaribishi sana. Ninajisikia nyumbani sana, mpaka nimehubiri hata nikapwelewa na sauti.

⁵⁰ Sasa, Ndugu Ned Iverson ataziendeleza ibada baada yangu, huko chini Co—Columbia, huko chini pamoja na Ndugu Bigbee. Ndugu Ned, upo hapa ndani, usiku wa leo? Sijui kama... Naam, huko nyuma. Mpresbiteri, aliyejazwa na Roho Mtakatifu. A-ha.

⁵¹ Naye Dk. Lee Vayle na mke wake, marafiki wa thamani, wapendwa wangu. Ndugu Vayle amefanya kazi pamoja nami katika mkutano, rafiki wa thamani. Nadhani watu hawa wote wametambulishwa na kadhalika. Upo hapa, Ndugu Vayle? Uko humu jengoni, usiku wa leo? Huko nyuma. Bwana akubariki. Dada Vayle, uko wapi? Sikufanya zaidi ya kukupungia mkono. Mungu akubariki, dada. Tuna furaha sana kuwa nao wote hapa.

⁵² Nanyi nyote mniombe sasa. Nami ninatembea tu kwa imani, nikiamini ya kwamba, karibu wakati wowote, huenda tukakuona kule Kuja kwa Bwana. Sijui jinsi gani, wakati gani, mahali gani, bali ninataka kuwa tayari atakapokuja. Na wakati mwingine huenda nikawazia huenda ikawa ni *hivi*, na huenda ikawa ni vinginevyo. Lakini, kwa vyovyote vile, ninataka kuwa pale Yeye atakapokuja. Ninataka kwenda pamoja na Yeye. Sasa, hiyo ndiyo shauku yangu. Na si kwamba tu ninataka kwenda; ninataka marafiki wangu wote, pia nataka adui zangu wote, waende, pia. Namtaka kila mtu aende.

⁵³ Nilikuwa na ono dogo, ama, sitaki kuliita kuhamishwa. Kamwe sikuwa nimepata ono kama hilo. Nilikuwa nimesimama kule juu nikiliangalia, nikijiangalia mwenyewe, hapa hivi majuzi. Wengi wenu mlilisoma kwenye magazeti na kadhalika. Enyi marafiki, ha—hamwezi kuthubutu kukosa hilo. Kamwe msifanye hivyo.

⁵⁴ Sasa, kuna mahali fulani kule. Nilikuwa huko kama tu nilivyo hapa, nikijiangalia mwenyewe. Nimekuwa na maono.

Ninajua maono ni nini. Kama hilo lilikuwa ni ono, lilikuwa ndilo la kigeni kuliko yote niliyowahi kuwa nayo. Nami nikawaona wale watu, wale ambao wametuaacha. Niliwaona kule. Wazee walikuwa ni vijana. Nao walikuwa wamesimama pale, wanadamu kama tu nilivyo mimi, ila tu wasio na dhambi. Ilikuwa ni zaidi ya ukamilifu. Adhimu! U—usingeweza kabisa kutaja kile kilichokuwa.

⁵⁵ Ndipo nilipojua ya kwamba ilinibidi kurudi, kulikuwa na jambo moja tu, hilo, ningerudi, kujaribu kuwashawishi watu. Chochote ufanyacho, usipakose. Msipakose. Usipakose. Hamwezi kuthubutu kupakosa. Kila kitu kingine, acha kila kitu kingine kiende, bali uwe tayari kwake, mnaona, chochote ufanyacho.

⁵⁶ Nitakuwa nikienda kwenye huduma za kimishenari sasa, Bwana akipenda, majira haya ya baridi kali, nitakaporudi kutoka kwenye ziara hizi, kwa hiyo niombeeni. Kwa sababu, hapa ni rahisi, mara moja moja unamwona roho mchafu akiingia mkutanoni na kujaribu kusumbua. Lakini katika sehemu hizo, hao ni wachawi na ibilisi. Afadhali ujue unachonena habari zake. Hakika ilibidi. Maana, hao ni pepo, nao watakupa changamoto kotekote. Lakini, loo, jinsi, hapana wakati mmoja...Ninasema hilo mkono wangu ukiwa hapa kwenye Biblia yangu. Hakuna wakati mmoja, nanyi mnajua mnaweza kuwazia ni mara ngapi kote ulimwenguni limepewa changamoto, ila kwamba Mungu alijitokeza jukwaani na kulivuta lile pazia nyuma, na kujionyesha Mwenyewe, Mungu, kama tu alivyokuwa katika wakati wa Eliya. Yeye angali ni Mungu. Naam. Si hata wakati mmoja. Hiyo ndiyo sababu mimi...

⁵⁷ Baadhi yenu, baadhi ya wahudumu, wanakuja na kuniomba nije kwao. Ninangojua mpaka ninapojisikia kuongozwa kwenda. Ndipo kama nikija, ninakuja tu katika jina langu mwenyewe, nikija jinsi hiyo, nipate tu kuwa rafiki yako. Lakini ninapojisikia kuongozwa kuja, basi ninaweza kuja katika Jina la Bwana Yesu. Ondoa miguu yako kwenye ndege hiyo, ni yangu. Amina. Ninaimiliki yote, katika Jina la Yesu Kristo. Basi utakutana na Yeye huko nje basi, kwa sababu wewe ni balozi wa Mungu basi. Lakini sasa, wakati kanisa fulani linapokutuma, ama, rafiki fulani akikuita, kitu fulani, unaenda tu, ukidhanja tena. Jamani, kudhanja! Nafikiri mmechoshwa na kusikiliza hilo.

⁵⁸ Sasa hebu tuifungue Biblia ya kale yenye neema. Na kabla hatujafanya hivyo, hebu tuombe. Mnaona, tunazungumza, na—na kadhalika, na sasa hebu na tuelekeze nia zetu Kwake sasa kwa dakika chache zijazo.

⁵⁹ Baba yetu wa Mbinguni, tulikuwa tukiwashukuru watu kwa ajili ya wema wao, na hisia zao kuu, zenye ukarimu kwetu, na jinsi tunavyowathamini. Na sasa, Baba, tunataka kukushukuru

Wewe, juu ya yote, kwa kuwa ni Wewe, Bwana, uliyefanya hili. Ni Wewe uliyetubariki na kuturuhusu kuketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo. Shetani angaliukatiza na—na kuuharibu mkutano wetu. Lakini Wewe ulitupenda vizuri sana, mpaka Wewe ukaturuhusu tu kukusanyika pamoja na kuwa na ushirika kwenye Neno. Nasi tunalithamini hilo sana, Mungu. Ingawa kidogo nimepwelewa na sauti kutokana na kuitumia sana sauti, Bwana, nilikuwa tu na wakati mzuri sana, nikimhisi Roho Wako akiibariki nafsi yangu. Neno, pasipo kupungukiwa na kitu, likitiririka tu kama mito, mpaka inanilazimu tu kuketi chini. Mungu, ninashukuru sana kwa jambo hilo.

⁶⁰ Pia jalia Ndugu yetu Parker, na wafanya kazi wake wote, na mahali hapa palipotualika, Bwana, naomba wabarikiwe. Wape maelfu ya nafsi. Sikia, wanapowaombea wagonjwa. Yasikie maombi yao, Bwana, na uwaponye wagonjwa. Na wanapojaribu kufanya jambo fulani katika Jina Lako, liheshimu, Bwana. Wape tunda la Roho. Na ninii... Pia wape ile shauku kuu ya moyo wao, Bwana, nafsi kwa ujira wao. Jalia, kwenye Siku ile tutakaposimama huko mbele Yako, jalia watu watoke kila mahali, wakimkumbatia mtu huyu wa thamani, mtauwa pamoja na wafanyakazi wake, “Kama usingalikaa hudumani, Ndugu Parker, tusingekuwa hapa.” Ee Mungu, tunajua hiyo ndiyo shauku aminifu ya mtumishi yeyote wa kweli wa Kristo, kujua kwamba wanaweza kuwaongoza maskini wanadamu waliopotea, kwa Kristo anayeokoa. Asante kwa hayo yote.

⁶¹ Na sasa, Bwana, tunaomba sasa ya kwamba utambariki kila mmoja. Na uibariki mikutano ijayo, kila mahali. Nenda na kila makazi. Kuwa pamoja nao tunapoondoka, usiku wa leo, kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali. Kuwa pamoja nasi njiani. Kaa kwenye gurudumu. Mweke adui mbali nasi, Bwana. Nami naomba ya kwamba Wewe utayajalia mambo haya.

⁶² Sasa utupe shauku ya mioyo yetu, kila haja, usiku wa leo. Na yangu, Bwana, ni kwamba utaumega Mkate wa Uzima kwetu tena, usiku wa leo. Wakiwapo watu hapa wasiookoka, waokoe. Wowote wanaohitaji Roho Mtakatifu katika ubatizo, jalia aje usiku wa leo. Wagonjwa wowote; waponye. Yeyote aliye mchovu; wape furaha. Tujalie, Bwana. Libariki Neno Lako sasa tunapolisoma, na jalia Mwandishi atupe muktadha wake. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁶³ Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, 35 hadi 41, ningetaka kusoma Maneno haya ya thamani.

Ndipo tena siku ya pili yake Yesu alikuwa amesimama pamoja na wawili katika wanafunzi wake;... (Samahani)... Yohana alikuwa amesimama pamoja na wawili katika wanafunzi wake.

Akamtazama Yesu akitembea, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu!

Wanafunzi wawili, wale wanafunzi wawili wakamsikia akisema, wakamfuata Yesu.

Yesu aligeuka, akawaona wakimfuata, akawaambia, Mnatafuta nini? Wakamwambia, Rabi, (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi?

Akawaambia, Njoni, nanyi mtaona. Nao wakaenda, wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile: kwa kuwa ilikuwa yapata saa kumi.

Mmoja wa wale wawili waliomsikia Yesu ama... Yohana akinena, na kumfuata, alikuwa ni Andrea, nduguye Simoni Petro.

Huyo amwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia, Tumemwona Masihi, maana yake, Kristo.

Akampeleka kwa Yesu. Naye Yesu akamtazama akasema, Wewe u Simoni, mwana wa Yona: nawe utaitwa Kefa tafsiri yake Petro, au Jiwe.

⁶⁴ Sasa Mungu na aongeze baraka Zake kwenye Neno hili. Sasa, nataka kutoa, usiku wa leo, Bwana akipenda, kwa ajili ya maskini ne—neni moja, maneno mawili ninayotaka kutumia kutoka hapo. Maneno hayo mawili ninayotaka kutumia ni “kuhusika” na “kushawishika.”

⁶⁵ Sasa, kama tujuavyo, nasi sote tunajua, kwamba sasa tunaona kupoa kukuu, kote katika mataifa. Nilipoanza, kulikuwako na mikogo mingi juu ya mkutano. Watu walikuwa katika mikutano ya maombi, kila mahali. Kukosolewa, magazeti yalinikosoa. Mwanamke mmoja aliendesha maili elfu tatu kwa tekisi, apate tu kuhudhuria mkutano Canada. Hawahusiki hivyo tena. Inaonekana kana kwamba kumekuwa na ukengeufu. Na inaonekana kana kwamba hakuna kuhusika sana, si sana, kwa vyovyote vile, si kama vile wanavyopaswa kuwa. Kuhusika kidogo sana.

⁶⁶ Sasa, karibu kuhusika pekee tuliko nako, sio mikutano hiyo ya usiku kucha. Wakati, ni—nilipokaa jukwaani wakati mmoja siku nane usiku na mchana, pasipo kuondoka, nikijaribu kuwaombea watu wote. Na hatimaye, kulikuwako na watu elfu arobaini na kitu walingojea kuombewa. Mnaona? Nisingeweza kufanya hivyo. Lakini wangelipeleka kundi *huku*, na kuenda mwituni; wangepeleka kundi *huku*, waende mwituni; wahudumu wakiwaombea watu hata wakapata ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wasingepumzika kamwe mpaka walipompokea Roho Mtakatifu.

⁶⁷ Samahani. Nilisema elfu arobaini na mbili. Ninaamini, mngeweza kuliangalia lile gazeti, walikuwa elfu ishirini na nane, ndivyo walivyokuwa, ambao walikuwa wangali walingojea. Kwa maili kadhaa kuzunguka Jonesburg, hapakuwapo hata na

mahali ambapo ungeweza kukodi. Na kusimamisha mahema mijini, na kila kitu. Hawahusiki hivyo tena. Mnaona? Mioto ya uamsho inafifia.

⁶⁸ Kuhusika, kwa sasa ni, “Njoo tu ukajiunge na kanisa.” Ama, kuhusika kukuu ni, “Isaidie huduma fulani ya redio, ama kipindi fulani cha televisheni, na kulifanya namna fulani ya maonyesho,” na kwa—kwa manufaa, bila shaka, hakika. Mijengo mikubwa, kujenga shule kubwa kubwa, na kadhalika, namna hiyo. Inaonekana ndiko ku—kuhusika sasa. Kidogo walipoteza ono la maombi hayo na kushawishi, kama waliyokuwa nayo. Kuna jambo fulani limetukia. Ningetaka tu kujua lilikuwa ni kitu gani. Na sasa hawaonekani kuhusika.

⁶⁹ Unaweza kulitembelea kanisa *hili*, ama kuwaalika watu waje madhabahuni, na ilikuwa kwamba wangekimbia tu madhabahuni. Nami nimeona ule wakati nilipokuwa nikihubiri, kabla hata sijamaliza mahubiri yangu, madhabahu na huku na huku kwenye marefu ya kanisa kungejaa watu. Nimeona wakati ambapo Roho Mtakatifu angeenda kwenye kusanyiko, na—na kubashiri na kumwambia mtu fulani kitu fulani, nao watu wangeshangaa mno na kuzirai papo hapo kitini mwao.

Kuna kasoro mahali fulani.

⁷⁰ Ningali ninafanya jambo lile lile. Ingali ni Injili ile ile. Kamwe sijaibadilisha hata kidogo tangu nilipoanza. Nilianza tu na Neno wazi, dhahiri la Mungu, nami nikadumu moja kwa moja juu Yake, tangu wakati huo. Miaka thelathini na miwili nimekuwa nyuma ya mimbara, wala kamwe sijaghairi wala kubadilisha lolote; nimeliweka jinsi tu nilivyoanza. Siwezi kulighairi. Ni Neno la Mungu. Na—na kama nikilisema jinsi tu limesemwa *hapa*, wakati huo mwingine inanibidi kusema jambo lile lile, maana *Hivi* ndivyo Hilo lilivyoandikwa hapa. Mnaona? Kwa hiyo, kamwe siwezi kufanya lingine lolote kulihusu. Naye Roho Mtakatifu angali anafanya jambo lile lile.

⁷¹ Kwa hiyo, lakini inaonekana kana kwamba hakuna kuhusika vya kutosha. Sasa mimi... sijui kwa nini, kwa nini hakuna kuhusika kama kulivyokuwa? Ni, ninaamini sababu ya kutokuwako na kuhusika kadiri kulivyokuwa, hawajashawishika kama walivyokuwa. Huna budi kushawishika kabla ya kuweza kuhusika.

⁷² Huhusiki, unauchukua wakati sasa, badala ya kufanya uinjilisti na kujaribu kufanya jambo fulani, kila mtu anataka shule kubwa mno, ama kitu fulani kikuu mno wanachoweza kufundisha, na—na kuwafanya wahudumu wawe na adabu bora zaidi za mimbarani na kadhalika.

⁷³ Mnajua ninaloamini? Ninaamini ya kwamba watu hawajashawishika ya kwamba Yesu yuaja karibuni. Siamini kwamba wameshawishika kwamba Yeye anakuja kwenye wakati huu. Nami ninaamini hiyo ndiyo sababu hawahusiki, kwa

kuwa hawajashawishika kikamilifu. Kweli. Hawajashawishika kwamba Yeye yuko pamoja nao. Kama walishawishika, wangerudi kwenye Neno. Hiyo ni kweli. Na sasa huenda watu wengi wakalielewa vibaya.

⁷⁴ Upendo, upendo ni—ni nidhamu. Inakubidi kuwapa watu nidhamu, kama unawapenda. Kama msichana wako mdogo alikuwa ameketi huko nje barabarani, kama nilivyosema asubuhi ya leo, akifinyanga keki za matope; kama kweli unampenda, utamwondoa hapo barabarani.

⁷⁵ Vipi kama mke wako alisema... Yohana *Nanii*, vyovyote jina lako lilivyo, unajua, unamwacha tu azurure na wanaume wengine, kwa sababu ulisema, “Nautakia heri maskini moyo wake! Yeye anataka kufanya hivyo. Nami ninampenda sana, nitamwachilia afanye hivyo.” Ungekuwa mume duni sana. Anapaswa kukufukuza, na kumpata mtu anayempenda, atakayemshughulikia. Sikulimaanisha hivyo, maana huwezi kufanya hivyo.

⁷⁶ Lakini ninajaribu kusema nini? Ni hivi, kwamba, vipi kama Mungu angalimwambia Hawa, “Maskini Hawa. Unajua, wewe ni mtoto Wangu. Ni—ni—ni... Hukumaanisha kufanya hivyo”? Hakika, hakumaanisha kufanya hivyo. Bila shaka, hakumaanisha. Bali alilifanya. Nasi tunajua alilifanya. Tungali tunaona matokeo yake. Lakini, mnaona, Yeye—Yeye alimpenda, na Yeye—Yeye ilimbidi kulitimiza Neno Lake kwake.

⁷⁷ Naye Mungu hana budi kulitimiza Neno Lake kwetu, kwa hiyo hatuna budi kulitii Neno Lake. Ndipo tunapolitii Neno Lake, na kumwona basi akithibitisha yale aliyosema angefanya, basi tunashawishika, kweli, kwamba Neno ni la kweli. Sasa, tunapoona, tunaleta... .

⁷⁸ Hapa sio muda mrefu uliopita, mwinjilisti huyu mashuhuri kwa Mwislamu, mlisoma hayo gazetini, kama nilivyofanya. Mwislamu huyu alimpa changamoto mwinjilisti huyo, kwamba, “Yesu Kristo ilikuwa ni kumwabudu mwanadamu; kwamba watu walikuwa wakimfuata mwanadamu.” Alimwamini Mungu yeye yule huyo mwinjilisti aliyemwamini, lakini kasema, “Yesu siye Mwana Wake. Ni ibada tu ya kujibunia ya wanadamu.” Basi huyo mwinji-... Yeye alimpa huyo mwinjilisti changamoto, kasema, “Bi—Biblia ilisema kwamba kazi alizofanya Yeye, Kristo, wafuasi Wake watafanya zile zile.” Akasema, “Sasa, nitawaleta wagonjwa thelathini, nawe uwaleta wagonjwa thelathini, nami nitaponya mmoja kila wakati ukimponya wako.” Mnaona? Ndipo huyo mwinjilisti akatimua mbio. Akatoroka.

⁷⁹ Basi kama ningalikuwa huyo mwinjilisti, ninaamini, iwapo sikuwa na imani ya kutosha kufanya hivyo, kamwe nisingalimruhusu asiyeamini huyo kusimama pale. Ningalisema,

“Ninajua mtu fulani katika milki yetu aliye na imani ya kulifanya.”

⁸⁰ Kwa nini? Inakupasa kushawishika, kwanza, kwamba ni Mungu, ndipo unajua mahali unaposimama. Ni kweli. Kushawishika, kwanza, ndipo unahusika. Ingawa watu wanadai kwamba Mungu yu pamoja nao, lakini wao... Si wote... Mama alizoea kusema, “Matendo hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno.” Hakika, yananena. Huna budi kutenda kazi, kuamini, kushawishika, ndipo basi utahusika.

⁸¹ Yesu alisema, “Ukinipenda Mimi, walishe kondoo Wangu.” Sasa, hapo ndipo ninapowazia tumekosea sana, ni kuwalisha kondoo Wake. “Ukinipenda Mimi, walishe kondoo Wangu.” Leo hii, karibu ni, “Wanyoe kondoo wangu.” Unawafikisha mahali na kuchukua kila kitu walicho nacho, na kuwafanya waweke dhamana makazi yao, na malipo yao yote ya uzeeni, na kila kitu kingine. Nena kuhusu kukata manyoya! Yesu kamwe hakusema hivyo.

Ndugu Parker alisema, asubuhi ya leo, “Mungu anawapenda watu Wake.”

⁸² Anawapenda kondoo Wake. Yeye alisema, “Walishe.” Nao kondoo hawana budi kupata Chakula cha kondoo. Wala Yeye hakusema, “Waelimishe kondoo Wangu.” Yeye alisema, “Walishe,” sio kuwaelimisha. “Walishe. Wape Chakula cha kondoo.”

⁸³ Chakula cha kondoo ni nini? Ule Mkate wa Uzima. Yesu ndiye Mkate wa Uzima, Injili, Kweli. Lihubiri pasipo kupatana. Ndipo unajua ya kwamba itakapokubidi kujibu kwenye ile Siku ya Hukumu kwa ajili ya nafsi yao, kama mhudumu wa Injili unaweza kusimama na kusema, “Hilo ndilo lililoandikwa kwenye Neno.” “Walishe ile Kweli. Lisha kondoo Wangu.”

⁸⁴ Wakati Yohana alipohusika sana, kwamba alijua Masihi alikuwa akija katika wakati wake. Yohana Mbatizaji alijua hilo, kwa hiyo alijua kwamba Masihi angekuja katika wakati alimoishi. Lakini wakati alipotoka nyikani, kamwe hakuanzisha shule zozote. Hakuanzisha vyo vyovyote. Kamwe hakuanzisha madhehebu yoyote. Kwa nini? Yeye alishawishika kwamba Masihi angekuja katika wakati wake. Chakula chake, Ujumbe wake, matendo yake, yalishuhudia hilo.

⁸⁵ Nasi tunaamini kwamba Yeye Yuaja katika wakati huu. Kwa nini tunataka kuhodhi kitu kikubwa? Kwa nini tutake kufanya hivyo, kujenga mamilioni ya dola katika shule na majengo, na halafu kusema Yesu anakuja? Mbona, umma unajua vema zaidi ya hilo. Wanajua unazungumzia jambo ambalo huliadini. Tuweke katika matendo tunayohubiri. Kweli. Sasa hatuna budi kufanya hivyo.

⁸⁶ Yohana alikuwa na hakika sana. Wakati alipozaliwa, yeye alijua alizaliwa kwa njia ya kipekee.

⁸⁷ Sote tunajua jinsi Zekaria alivyomwona Malaika. Na hilo hapana shaka lilikuwa ni gumu sana kwa huyo mume na mke wazee. Zekaria alikuwa ni mtu mwenye umri mkubwa, naye Elisabeti alikuwa ni mwanamke mkongwe, bali walikuwa wameamini ya kwamba—ya kwamba Mungu siku moja angewapa mtoto mchanga. Alikuwa ni tasa. Nasi tunajua Yohana alipozaliwa, kuzaliwa kipekee, huku akijua kwamba angekuwa mtumishi wa Mungu, hapana shaka lilikuwa ni jambo gumu kwa huyo mume na mke wakongwe. Kwa kuwa wanajua, kulingana na wakati wa maisha, kamwe hawangeishi kumwona mvulana huyo akiingia katika huduma yake.

⁸⁸ Naye baba wa Yohana alikuwa ni kuhani. Lakini badala yake, akiwa na wito huo, kuenda huko chini kwenye seminari ambako baba yake alitoka, asingeweza kushuka kwenda kule. Asingeweza kubahatisha kwa hilo. Kamwe asingejichanganyisha nalo. Kwa sababu, yeye aliona kwamba, katika Maandiko, yeye alikuwa awe, “sauti ya mtu aliaye nyikani.” Aliona kwamba yeye alikuwa awe, “Mjumbe ambaye angemtangulia Masihi.” Naye hana budi kuwa na hakika nalo. Basi alingojea nyikani hata akashawishika, ndipo basi akahusika. Alishawishika. Alitaka, Yeye alitaka kukaa. Alikuwa na hakika sana nalo, kwamba angemwona Yesu, hata akasema hivi, “Hapo, Yeye amesimama miongoni mweni sasa. Huyu hapo Mtu miongoni mweni, Ambaye hamumjui.” Loo, ninapenda hilo!

⁸⁹ Yupo Mtu miongoni mwetu, usiku wa leo, bali nina furaha sisi tunamjua. Nami ninaamini Yeye Ndiye anayeshuhudia. Roho Mtakatifu mkuu anashuhudia kwamba Yesu yuaja karibuni, kwa maana ni kulingana na Neno, nazo ishara zote zinatimizwa. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

⁹⁰ Yeye hakutaka kusema habari Zake, kufanya kosa lolote, kwa hiyo alikaa nyikani mpaka akashawishika ya kwamba angejua Masihi alivyokuwa. Naye Mungu alimwambia ni ishara ya jinsi gani atakayoangalia, wakati atakapomwona Masihi. Kwa hiyo wakati alipomwona, na akaona ishara iliyopaswa kumfuata, alishawishika ya kwamba huyo alikuwa Ndiye. Akasema, “Ninashuhudia kwamba huyo Ndiye.” Kwa kuwa, Mungu, Ambaye alikuwa amemwambia, na kumtabiri kwa nabii, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, “Alikuwa ndiye sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito Yake.’” Ndipo Mungu ambaye alikuwa amemchagua tangu zamani, na kumkusudia tangu zamani kwa hiyo kazi, yeye alimngojea Mungu huyo mpaka akasikia kutoka kwa huyo Mungu. Amina. Wakati Mungu huyo alipomwambia litakalotukia, alishawishika. Wakati alipoiona huyo ishara, alisema, “Huyo hapo.” Amina.

⁹¹ Laiti tungalikuwa tu waaminifu hivyo! Kama tungengojea madhabahuni, sio kupata namna fulani ya hisia ndogo na

kuruka juu na kutoroka, bali kukaa pale. Haijalishi ni jambo gani linalotukia, dumu pale mpaka umeshawishika kikamilifu kwa nguvu za kufufuka Kwake, kwamba Roho Mtakatifu amekushika na anakushikilia, nawe ni kiumbe kipya katika Kristo. Dumu pale mpaka umekufa na kufufuka tena, ndipo hutaenda majini mnafiki. Utaenda kule, nawe unajua kwamba Yeye—Yeye alikufa kwa ajili yako, nawe ukafa pamoja na Yeye. Sasa unashuka chini, upate kufufuka pamoja na Yeye tena; kuonyesha ulimwengu kwamba unaamini Yeye alikufa na kufufuka tena, nawe umekufa pamoja na Yeye, na tayari umefufuka tena. Na sasa utaketi katika mahali pa Mbinguni, ukila Chakula cha kondoo. Kweli.

⁹² Andrea, huyu mkuu tunayenena habari zake, ndugu yake Simoni, yeye alikaa usiku kucha, mpaka akashawishika. Wakati alipokuwa akipitia ufukoni, Yohana, nabii huyu mkuu aliendelea kusema, “Yupo Mtu! Wakati umekaribia. Enyi nyote vizazi vya nyoka nyasini, msiwazie kusema, ‘Mimi ni mfausi wa *hili*, na ni mfuasi wa *lile*. Tunaye Ibrahimu kama baba yetu.’ Nitawaambia, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Loo, yeye alikuwa akiliweka tu wazi, shoka kwenye shina la mti.

⁹³ Mnaona, Yohana alikuwa ni mtu wa nyikani. Angalia yale aliyozungumzia: mashoka, miti, nyoka. Mnaona? Hayo ndiyo aliyoyazoea, huko nje nyikani. Naye akasema, “Shoka limewekwa kwenye shina la mti, na kila mti usiozaa tunda zuri utakatwa na kutupwa chini na kuchomwa.” Kugonga mti kwa shoka; kuvikata vichwa vya nyoka, na kadhalika. Yeye alikuwa ni mtu wa nyikani.

⁹⁴ Si ajabu Yesu alisema, “Mlitoka kwenda kuona nini?” Ile *Heri Iliyosahauliwa*, kama nilivyohubiri juu yake. Wakati alipovuka kilima, wanafunzi wa Yohana walisema. “Mlitoka kwenda kuona nini, mtu aliyevikwa mavazi mororo?” Akasema, “Hao ndio wa aina wanayoita, ‘Daktari, baba mtakatifu.’ Nao wanavaa nguo nyororo. Wanawabusu watoto wachanga, na kuwaoza vi—vijana, na kuwazika wazee. Yeye hutumia kisu cha mfukoni.” Mtu kama huyo angejua nini kuhusu Upanga wenye mikono miwili huko kwenye mstari wa mbele wa vita? “Mlitoka kwenda kumwona mtu?”

⁹⁵ Baadhi yao walisema, “Basi mlitoka kwenda kuona unyasi unaotikiswa na upepo wowote, ama kundi lolote dogo linaloweza kujitokeza, liwabadilishe kutoka *hili* kuwa *lile*, na *hili* kuwa *lile*?” Sio Yohana. Yeye alishawishika. A—alijua ambapo alikaa. Alijua mahali pake. Hawakuwa wakimtikisa Yohana huku na huku. La, la.

⁹⁶ Kasema, “Mlitoka kwenda kuona nini basi, nabii?” Akasema, “Nami nawaambia, mkuu kuliko nabii. Yeye ni zaidi ya nabii.”

⁹⁷ Kwa hiyo Yohana alishawishika, naye akaanza kuhubiri. Basi Andrea alikuwa akihudhuria mikutano. Na kwa hiyo wakati Yesu alipopitia pale, naye Andrea na mwanafunzi mwingine walikuwapo, basi Yohana aliwaelekezea, na kusema, "Tazameni Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu." Nao wakamfuata.

⁹⁸ Ninapenda hilo. Laiti ningalikuwa na nguvu kama hizo katika kuhubiri kwangu. Nikisema, "Tazameni Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu," na kila mtu angemfuata. Jamani! Hebu mimi . . .

"Ninampata wapi, Ndugu Branham?" Ninaweza kuwaonyesha.

⁹⁹ Sio muda mrefu uliopita, nilikuwa katika mkutano wa Wafanyabiashara. Nami nilikuwa nikihubiri kwenye Pwani ya Magharibi. Ndipo palikuwapo na jamaa aliyenijia, na kusema, "Aisee, kwani wewe si mhubiri?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Unafanya nini na hawa wafanyabiashara?"

Nikasema, "Mimi ni mfanyabiashara."

Naye akasema, "Kwani unafanya biashara ya aina gani?"

Nikasema, "Biashara ya hakikisho."

Yeye akasema, "Bima ya aina gani?"

Nilisema, "Hakikisho."

Kasema, "Ni ya aina gani?"

¹⁰⁰ Nikasema, "Hakikisho lililobarikiwa, Yesu ni wangu." Nikasema, "Kama unataka hati ya mkataba, ningetaka kuizungumzia pamoja nawe."

¹⁰¹ Rafiki yangu, Bw. Snyder, mvulana wa thamani, alikuja nyumbani kwangu. Nami nilimjua nilipokuwa jamaa mdogo, na tulienda shuleni pamoja. Akasema, "Billy, ningetaka kukuuzia bima."

¹⁰² Vema, nilifanyiwa utapeli wakati mmoja, juu ya bima, nami kamwe sikuichukua tena. Kwa hiyo akasema . . . Nikasema, "Wilmer, hakika ni—ningeninii . . . ninakupenda, bali," nikasema, "tayari ni—nina hakikisho."

Akasema, "Loo, ati unayo?"

¹⁰³ Mke wangu akaniangalia kana kwamba nilikuwa ni mnafiki. Alijua sikuwa na bima yoyote, bali nilisema, "hakikisho." Mnaona?

¹⁰⁴ Akasema, "Loo, samahani, Billy." Akasema, "Ni ya kampuni gani?"

Nikasema, "Uzima wa Milele."

Kasema, "Siamini nimewahi kusikia juu ya kampuni hiyo."

Nikasema, “Unapaswa kuisikia.” Loo, nimeshawishika ni ya kweli. Ni ya kweli.

105 Kwa hiyo, Yohana alihubiri na kusema, “Huyo hapo, Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.”

106 Ninapomwona akienda kupitia kwenye kusanyiko, anamvuta mwenye dhambi, ama mgonjwa, na kuzungumza nao, na kujua kwamba Huyo ndiye Mungu yule yule. Na mtu yeyote, angaliweza kujua lolote, angejua kwamba mimi nisingeweza kufanya hilo. Ningetaka kusema, “Tazameni Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.”

107 Ninapenda watu, waseme, “Ninaamini hilo. Sasa ninazitubu dhambi zangu. Ninamwamini Yesu Kristo.” Loo, ninapenda kuwaona wakifanya hivyo.

108 Nao wanafunzi hawa wakamfuata Yesu mara moja. Naye akaangalia huku na huku. Akawaona. Ndipo akasema, “Mnatafuta nini?”

109 Wakasema, “Rabi,” maana yake, “Bwana, unakaa wapi Wewe?”

110 Akasema, “Njoni mwone.” Sasa huo ni mwaliko mzuri sana. “Njoni mwone.” Napenda hilo.

111 Hivyo ndivyo Filipo alivyomwambia Nathanaeli, wakati Nathanaeli aliposema, “Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?” Yeye akasema, “Njoo uone.”

112 Kwa hiyo basi, njoo, uone. Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo, uone. Mnaona? “Njoo, ujionee mwenyewe.”

113 Sasa, wao walisema ilikuwa ni wakati wa jioni, kwa hiyo Andrea alikesha usiku mzima. Loo! Hiyo ni njia nzuri. Alikaa mpaka akashawishika. Yale Mtu huyo aliyokuwa amemwambia usiku huo, yale aliyokuwa amemwambia, ama yale aliyofanya, kulikuwako na jambo fulani ambalo kabisa lilimshawishi Andrea kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

114 Kesho yake mapema sana, ninawazia, yeye alilinyakua koti lake na kofia, akaanza kuteremka, maana Petro alikuwa akienda kuvua samaki mtoni. Ndipo akasema, “Njoo, uone Mtu tuliyempata. Ndiye Masihi.” Alishawishika. Wakati aliposhawishika kikamilifu kwamba alikuwa ni Masihi, alihusika kuhusu ndugu yake.

115 Hiyo ndiyo shida, usiku wa leo. Watu hawajashawishika juu ya Ujumbe. Watu hawajashawishika juu ya Roho Mtakatifu. Kama kweli ukishawishika, basi unahusika. Utafanya kila uwezacho, kufanya lolote lile unalopaswa kufanya nalo. Wasema, “Vema, Ndugu Branham, mimi si mhubiri.” Vema, unaweza kufanya jambo fulani, pia.

116 Nakumbuka wakati mmoja nilikuwa na mkutano. Kulikuwako na mkulima aliyeokoka na kujazwa na Roho

Mtakatifu. Naye hakuwa na kitu ila ujuzi wake, na lori. Lakini yeye aliwabeba watu wengi sana akawapeleka mkutanoni, akawafanya thelathini zaidi kujazwa na Roho Mtakatifu, kabla ninii...?...Kwa nini? Alishawishika. Na wakati aliposhawishika, alihusika. Maskini binti yake akaponywa. Tulikuwa na wagonjwa kila usiku, lori zima lao, likiwaleta kutoka kila mahali. Thelathini wakampokea Roho Mtakatifu. Mnaona? Yeye alishawishika kwamba ilikuwa ni kweli, kwa hiyo alihusika juu ya mtu mwingine. Nasi tuna...Kama tumeshawishika ya kwamba Yesu yuaja karibuni, tutahusika juu ya watu wetu waliopotea. Tutakuwa tukifanya yote tuwezayo kuipeleka nje Injili.

¹¹⁷ Yakobo alikaa usiku kucha, usiku mmoja, akipiga mwereka. Huyu mtawala mpiga mwereka, alipiga mwereka usiku kucha. Alikuwa akimkwepa Esau *hapa* na *pale*. Alimwogopa kabisa, huyo. Ndipo akasikia Esau alikuwa anakuja. Akamvusha mke wake kile kijito. Akavuka ng'ambo ya pili akapiga magoti. Mwajua, Mungu alishuka akamshika Yakobo, nao wakashindana mwereka usiku kucha. Kwa hiyo ha—hakuwa ameshawishika kabisa, kwanza kabisa. Lakini wakati Mungu alipomaliza naye, alishawishika. Naam. Yeye alikaa na kushikilia mpaka akashawishika kwamba ilikuwa ni Mungu.

¹¹⁸ Ndugu, hakumwogopa Esau tena. Akavuka huo mto, naye alikuwa mnyonge na anachechemaa. Ndio wakati mbaya sana angalikuwa ndani yake, ilivyoonekana. A—alikuwa—alikuwa mnyonge kuliko alivyowahi kuwa. Alikuwa amelemazwa na kila kitu. Lakini Esau alimwambia, “Utaniruhusu nitume jeshi lije likusaidie?”

¹¹⁹ Kasema, “Hata sihitaji usaidizi.” Kwa nini? Alikuwa ameshawishika kwamba yule Mungu, aliyekuwa amemshika, angeweza kumshughulikia. Haleluya! Laiti watu wanalifanya tu hivyo.

¹²⁰ Kama unaweza kushawishika ya kwamba Mungu anayekushika, anayeutikisa moyo wako, anakufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Acha maradhi, kifo, ama chochote kingine kije, wewe umeshawishika Yeye anaweza kukutunza vizuri. Hakika. Amina. Ninapenda hilo.

¹²¹ Shamgari, maskini jamaa yule tuliyenena habari zake hivi majuzi usiku, yeye alihusika juu ya familia yake. Naam, alijua walikuwa na njaa. Ndipo Wafilisti wakapanda kule, elfu moja ya hao, ninaamini, mia sita na kitu. Ninaamini, mia sita wao wakapanda barabarani, watu wenye silaha. Yeye alihusika juu ya familia yake, maana wangeona njaa hata wafe kwenye majira hayo ya baridi kali. Lakini akakaa pale, akiwaza na kuchunguza. Angefanya nini? Alikaa pale mpaka akashawishika ya kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake.

¹²² Sasa, angalieni kile angaliwazia. “Sasa, hapa, baba yangu Ibrahimu, ambaye kwake ninayo mwilini mwangu alama ya tohara, kwa sababu kwamba ninaamini Ibrahimu alikuwa ni mtu wa Mungu. Yeye alishawishika. Akaondoka nyumbani kwake. Akaacha kila kitu alichokuwa nacho, akamtumikie Mungu. Ndipo juu ya mlima siku ile, wakati alipomtoa kondoo dume badala ya Isaka, Mungu alimwambia Ibrahimu, ‘Kwa sababu umefanya jambo hili, uzao wako utamiliki lango la adui.’” Hiyo ni kweli. “‘Uzao wako, Ibrahimu, ninakuahidi. Ninaapa kwa hilo.’” Haleluya! Loo, jamani! Sasa najisikia kubarikiwa. “‘Ninaapa kwa hilo. Ibrahimu, uzao wako utamiliki lango la adui wake.’”

Sasa Shamgari angeweza kusema, “Mimi ni uzao wa Ibrahimu.” Amina.

¹²³ Basi iwapo Shamgari angeweza kuliwazia hilo, akiwa ni uzao wa kawaida wa Ibrahimu, vipi kuhusu usiku wa leo, nasi ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu? Loo! Whiu! Mnafikiri mimi nina kichaa. Labda ninacho. Niacheni. Ninajisikia bora zaidi hivi kuliko nilivyojisikia nilipokuwa na akili hiyo nyingine. Naam. Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu! Kanisa ndilo Uzao wa Kifalme, ulioahidiwa. Basi iwapo uzao wa kawaida ungeweza kuchukua ujasiri kiasi hicho, Uzao wa Kifalme unapaswa kufanya nini, pamoja na—pamoja na Uwepo wa Roho Mtakatifu akitia mafuta kote, akijionyesha Mwenyewe? Whiu! Utukufu! Hakika.

¹²⁴ Shamgari alisema, “Mimi ni uzao wa Ibrahimu.” Naye akaanza kuliwazia, “Mungu alimwambia Ibrahimu, ninaamini hilo, kwamba uzao wake utamiliki malango ya adui wake. Nao hawa hapa, wakipita taratibu langoni pangu.” Akanyosha tu mkono, akachukua fimbo ya kuongozea ng’ombe. Sasa, yeye hakusimama.

¹²⁵ Kamwe hakungojea apate kujifunza namna ya kupigana, ama kusema, “Sasa ngoja kidogo. Mimi ni Uzao wa Kifalme. Mimi ni uzao wa Ibrahimu. Nimetahiriwa. Kwa hiyo, mwajua, Wafilisti hawa wote ni askari wa vita hodari. Wamekuwa wakifanya mazoezi kwa muda mrefu. Nitashuka niende kwenye seminari na kupata Ph.D. na L.L.D. zangu, nami nitajifunza jinsi ya kupigana. Nitajifunza katekisimo, kanuni zote za kanisa.”

¹²⁶ Kama angalikuwa amefanya hayo, hayo ndiyo yote angalijua lolote kuyahusu! . . . ? . . . [Kusanyiko linasema, “Hakika.”—Mh.] Angalijua tu hayo, basi asingaliwashinda. Halafu asingaliweza kumstahimili adui.

¹²⁷ Huwezi kumstahimili adui. Siwezi kumstahimili. Lakini ninakumbuka ninaishi chini ya ahadi, haleluya, ambapo tayari nguvu zake zimestahimiliwa hata na zaidi, na kushindwa, na kutupwa chini. “Mimi ni zaidi ya mshindi, sasa hivi.” Sio mimi mwenyewe, bali niko ndani Yake Yeye ambaye alinishindia, mnaona, na hilo laendelea kuishi. Mimi ni sehemu ya Uzao wa

Kifalme wa Ibrahimu. Liwazie kwa dakika moja, kisha uchukue fimbo yako ya kuongozea ng'ombe. Mfukuze ibilisi wa shaka kutoka kwako. Naam.

¹²⁸ Kasema, “Mimi...siwezi kujifunza kupigana.” Kama akifanya hivyo, hivyo ndivyo tu ajuavyo jinsi ya kufanya, ni kupigana tu. Hayo tu ndiyo angaliweza kuzungumzia.

¹²⁹ Leo hii, hivyo ndivyo tunavyojaribu kulifanya leo hii. Watu walisema, “Nina wito maishani mwangu kuwa mhudumu.”

¹³⁰ “Vema, sasa, mwanangu, nitamwita askofu, nami nitatafuta kujua kama siwezi kukuacha uende shuleni, nawe uweze kujifunza saikolojia, na kujifunza mambo haya yote. Na yapata miaka kumi katika seminari huenda ikakuandaa vizuri.” Hiyo itamwandaa, hakika kabisa. Litamwandaa hivi kwamba kamwe hataweza kusimama tena.

¹³¹ Ni tofauti jinsi gani ilivyo, kumtuma mhudumu leo, kuliko ilivyokuwa kwenye Kanisa la kwanza. Hawakungojea miaka kumi. Walingojea siku kumi. Kama ikikuchukua miaka kumi kushawishika... Wao walishawishika katika siku kumi. Amina. Huenda akashawishika kuhusu saikolojia, bali huna budi kupata elimumagoti. Siku kumi tu, walishawishika, kisha walihusika kuhusu hao wengine. Baadhi yao hata wasingeweza kutia sahihi jina lao wenyewe. Biblia ilisema walikuwa wasio na elimu wala maarifa, bali walishawishika. Haleluya!

¹³² Sijali juu ya elimu. Nimeshawishika kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Nimeshawishika Huyu ni Roho Mtakatifu. Nimeshawishika Yeye ni Mponyaji. Nimeshawishika Yeye ni Mwokozi. Nimeshawishika Yeye yuaja. Nimeshawishika *Hili* ni Lile. Nimeshawishika. Ninaliamini.

¹³³ Walisema wameshawishika. Jambo fulani lilitukia. Walishawishika, kisha wakahusika baada ya kushawishika. Walihusika kuhusu kulieneza Neno Lake kwa hao wengine. Hiyo ilikuwa ni ishara nzuri ya kwamba walishawishika: walihusika.

¹³⁴ Hawakuhusika kuhusu elimu, kuhusika kama wangeweza kusema “amina” vizuri tu. Hawakuhusika kuhusu dhehebu walilofuata, ama kama walikuwa na kadi ya ushirika, au la. Walishawishika kwamba yote waliyohitaji yalikuwa ni Yeye.

¹³⁵ Nami niko vivyo hivyo usiku wa leo. Nimeshawishika ya kwamba yote tunayohitaji ni Kristo. Hatuhitaji meya mpya. Hatuhitaji marais wapa. Hatuhitaji jeshi jipya. Hatuhitaji bomu jipya. Tunamhitaji Yesu.

¹³⁶ Hayo tu ndiyo wa—ndiyo waliyoshawishika kuyahusu. Nao pia waliamini ya kwamba Yeye angeninii... Walishawishika ya kwamba Yeye—Yeye angekidhi kila kitu walichohitaji.

Mmeshawishika hivyo, usiku wa leo?

¹³⁷ Semeni, “Nimeshawishika. Haijalishi ni nini kinachokuja mbele yangu, Yeye atakikabili. Haijalishi ni nini kinachokuja

mbele yangu, mimi nimeshawishika Yeye atanishughulikia. Alisema angefanya hivyo.”

138 “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Usiwazie juu ya kesho, itajishughulikia.” Hiyo ni kweli, wazia tu leo. “Kama Mungu alivika sana konde, na nyasi za kondeni, ambazo zipo leo, kesho hazipo; na kama Yeye aliwazia vya kutosha hata shorewanda asingeweza kuanguka mtaani pasipo Yeye kujua hilo,” ni zaidi sana vipi Yeye anajua kuhusu mahitaji yetu?

139 Nimeshawishika. Hiyo ndiyo sababu hamnioni nikiombaomba sadaka, na *hili, lile*. Nimeshawishika. Kama nikidumu na Neno hili, Mungu atadumu pamoja nami. Nimeshawishika. Sio lazima nipewe. Itakuja kwa njia fulani. Mimi, ni—nimeninii tu—nimeshawishika tu. Ninaliamini. Ninaamini kila Neno Yeye alilosema. Nimeshawishika Nalo. Nimeshawishika Yeye atakidhi haja zote nilizo nazo. Haitanibidi kuhofia juu yake.

140 Naye alishawishika pia kwamba hawakuhitaji lundo la saikolojia, na upuuzi huu mwingine wote, kuuchukua. Walishawishika ya kwamba hao waliokuwa...wa—waliowahubiria, ndio yote waliyohitaji, wangekuwa ndio yote waliyokuwa nayo.

141 Hiyo ndiyo shida yake siku hizi. Wanajaribu kushindilia upuuzi mwingine ndani yake, kanuni za imani, na vitu kama hivyo. Kamwe hujapata kushawishika kabisa kwamba Roho Mtakatifu ni wa kweli. Hayo tu ndiyo ninayohitaji. Hayo tu ndiyo anayohitaji. Hayo tu ndiyo mtu mwingine yeyote anayohitaji.

142 Nilikuwa huko Afrika muda sio mrefu uliopita. Walikuwa wakijaribu kuwaelimisha watu hao huko chini, na makabila. Nawe unapowaleta kwa mzungu, yeye anachukua dhambi ya mzungu. Anayo dhambi yake mwenyewe huko nje kwenye hilo kabila. Unamwingiza, anachukua dhambi ya mzungu, ndipo anakuwa maradufu mtoto wa kuzimu kuliko alivyokuwa, hapo awali. Jambo moja tu analohitaji. Yeye anamhitaji Kristo. Amina.

143 Hudson Taylor, wakati mmoja. Hamjasikia juu ya Hudson Taylor, yule mmishenari mashuhuri, Uchina? Palikuwapo na mvulana mdogo wa Kihindi. Akaokoka, akasema alikuwa na wito kwenye huduma. Akaja akamwambia Bw. Taylor, kasema, “Bw. Taylor, nichukue miaka minne ya saikolojia,” na mambo mbalimbali anayopaswa kufanya, “nayo itanichukua muda gani, kupata Shahada yangu ya Sanaa?”

144 Bw. Taylor akamwambia, kasema, “Mwanangu, kamwe usiuchome m—mshumaa wako nusu kabla hujaanza kwenda.” La.

¹⁴⁵ Hivyo ndivyo ninavyowazia, pia. Usingoje mpaka mshumaa umeungua nusu, na namna fulani ya shule imeshindiliwa ndani yako, namna fulani ya dawa ya kuhifadhi maiti. Usifanye hivyo. Bali ninasema, mara tu mshumaa ukiwashwa, anza. Sijaribu kuunga mkono ujinga, bali hili hapa ninalomaanisha. Kama hujui lingine lolote, waambie vile mshumaa ulivyowashwa. Hayo tu ndiyo wanayopaswa kujua. Waambie kilichouwasha huo mshumaa. Waambie kile kinachowaka mle ndani. Waambie tu jinsi ulivyowashwa. Acha nao wawashwe, wata—watayashughulikia hayo mengine. Bila shaka.

¹⁴⁶ Haikubidi kusema, kupitia katika namna zote za maneno makuu ambayo kwanza kabisa huyafahamu, wala hayana maana yoyote ukiisha kuyafahamu. Mnaona? Waambie tu, “Utukufu kwa Mungu! Roho Mtakatifu alinigusa, nami ni mtu tofauti.” Waambie jinsi huo mshumaa ulivyowashwa. Usingoje mpaka utakapoungua; halafu ni moshi wakati huo. Wengi sana wa hao siku hizi. Waambie tu jinsi ulivyowashwa.

¹⁴⁷ Yule kipofu ambaye Yesu aliyafungua macho yake kule juu, walikuwa kukawa na ubishi mkali juu yake. Mnakumbuka wakati alipopitia hapo, wale wanafunzi walisema, “Yupi aliyetenda dhambi, yeye au mama yake, baba yake?”

¹⁴⁸ Yesu akasema, “Si hata mmoja. Bali kwamba kazi za Mungu zidhihirishwe.” Naye akayafungua macho yake.

¹⁴⁹ Hawa hapa wakaja waandishi wote na Mafarisayo. Nao baba yake na mama yake waliogopa nusura kufa, kwa kuwa walikuwa tayari wamesema, “Mtu yeyote akimsikiliza Yesu huyo wa Nazareti, Nabii huyo, atakupatia tu barua kutoka kanisani. Umefukuzwa.”

¹⁵⁰ Hawajabadilisha hilo hata kidogo. Mnaona, ni wale wale! “Yeyote atakayemsikiliza, ama atakayeenda kwenye mkutano Wake, umeondolewa tu moja kwa moja kanisani, kwanza kabisa.” Wanalifuta jina lako moja kwa moja kutoka kwenye kitabu.

¹⁵¹ Kwa hiyo walienda wakamwona baba na mama yake, wakasema, “Huyu ni mwana wenu?”

¹⁵² Kasema, “Naam, ndivyo.” Kasema, “Tunajua huyu ni mwana wetu, na tunajua alizaliwa kipofu.”

“Vema,” kasema, “alipataje kuona?”

Kasema, “Ninyi mwulizeni. Ni mtu mzima.”

Kasema, “Mpeni Mungu utukufu. Mtu huyu ni mwenye dhambi.”

¹⁵³ Mbona, yeye asingeweza kubishania theolojia pamoja nao. Hasha. Bali kuna kitu kimoja alichojua. Alishawishika kwamba angeweza kuona. Kasema, “Kama Yeye ni mwenye dhambi ama si mwenye dhambi, sijui mimi. Sijui alitoka kwenye shule gani, wala lolote kuhusu hayo. Lakini hii ni hoja

moja nzuri ya kubishania niliyo nayo: ambapo nilikuwa kipofu, nimeshawishika kwamba ninaweza kuona; maana Yeye aliniambia ningeweza, nami nikamsikiliza.” Haleluya!

¹⁵⁴ Vivyo hivyo na mimi. Nilikuwa kipofu, bali sasa naona. Wakati mmoja nisingeweza kuliona Hili. Nilikuwa mwenye dhambi. Yeye akayafungua macho yangu. Ambapo nilikuwa kipofu wakati mmoja, sasa naweza kuona.

¹⁵⁵ Alikuwa na hoja nzuri ya kubishania, hakika alikuwa nayo, sana sana hata wasingeweza kumbishia wamshinde. Kwa nini? Alishawishika angeweza kuona. Naye alishawishika. “Hiyo,” yeye akasema, “ni ajabu sasa. Mnaweka, ninyi jamaa hapa, ndio viongozi wa dini wa taifa. Nanyi mnasema hamjui alikotoka Mtu huyu, na hapa Yeye anafanya mwujiza juu yangu, ambao haujawahi kufanywa ulimwenguni. Hilo ni jambo la kushangaza.”

¹⁵⁶ Ndugu, ninaamini yeye ni mwanatheolojia mzuri sana, kwa jambo hilo. Kwa nini? Alishawishika. Alikuwa na jambo fulani lililomshawishi. Alikuwa kipofu; angeweza kuona.

¹⁵⁷ Daudi, wakati alipokuja kwenye jeshi la Sauli, Goliathi upande huo mwingine, Daudi alikuwa ndiye mtu aliye mdogo kuliko wote wa kundi hilo. Goliathi alikuwa ndiye mkubwa kuliko wote. Sauli angekuwa akikaribia zaidi kulingana naye. Sauli alikuwa na yapata futi saba, nadhani, ama zaidi, labda nane, “Kichwa na mabega juu ya kila mtu jeshini mwake.” Naye Daudi alikuwa ndiye mtu aliyekuwa mdogo kuliko wote pale, naye alikuwa ndiye mtu pekee asiye funzwa pale. Lakini, ndugu, yeye alishawishika. Utukufu! Mnaona? “Ninapenda jinsi ninavyoonekana.”

¹⁵⁸ Tazameni. Yeye hakuwa amepata mafunzo. Hakuwa na mikuki. Hakujuu lolote kuihusu. Naye alikuwa tu ni maskini jamaa mwekundu. Lakini alishawishika, naye alihusika juu ya jeshi lililojiita “jeshi la Mungu aliye hai.” Naye alishawishika kwamba Mungu, Yule aliyekuwa amemsaidia na kombeo hilo, kumwua simba na dubu, hakika angeweza kumwondoa Mfilisti huyo asiyetahiriwa. Alishawishika, kisha akahusika kuhusu hilo jeshi. Haidhuru ni kiasi gani alipata... Kama umeshawishika basi unahusika, bali huna budi kushawishika, kwanza. Kwa hiyo, yeye alishawishika.

¹⁵⁹ Ninakumbuka usiku mmoja, usiku wenye joto kwelikweli, wenye kutisha kote kote, akienda vitani. Loo, mambo yalikuwa mabaya kwake. Ndipo akaomba. Alikuwa amelala huko nje chini ya mforsadi. Jeshi tayari lilikuwa tayari, huko nje kukabiliana naye. Yeye akalala chini ya huu mforsadi. Ndipo baada ya kitambo kidogo akasikia kitu fulani kikikaribia, nacho kikapitia kwenye vichaka vya mforsadi, na kutokea upande wa pili. Yeye akashawishika, ndugu. Haidhuru pingamizi zilikuwaje, yeye alishawishika kwamba Mungu aliingia ndani, akamtangulia.

¹⁶⁰ Enyi wanaume, kama mnaweza kusimama hapa, usiku wa leo, haijalishi mna shida gani; kama mnaweza kuhisi huo upepo unaoenda kasi wa Roho Mtakatifu ukipitia kwenu, na kusema, “Mimi ndimi Bwana niyaponyaye magonjwa yenu yote. Ninawaponya sasa.” Kama unaweza kushawishika, ndugu, hujali mawasiliano ni yapi huko nje, tayari unajua litatukia. Bila shaka.

Yeye alishawishika kisha akahusika.

¹⁶¹ Samsoni akisimama mbele ya Wafilisti, akiwa tu na mfupa wa taya la nyumbu mkononi mwake, hakuwa—hata hakuwa na silaha. Lakini alishawishika ya kwamba Mungu aliyemwinua, aliweza, kwa mfupa huo wa taya la nyumbu, kuwauwa hawa Wafilisti. Naye akawaua elfu moja.

¹⁶² Yule nabii mtoro, Musa, wakati Musa aliposhawishika ya kwamba ilikuwa ni Mungu kwenye kichaka kile. Mwajua, Musa kamwe hakuwa na ujuzi na Mungu. Alikuwa na theolojia nyingi sana. Lakini alikuwa ametoroka. Lakini wakati... Yeye alishawishika kwamba Huyu alikuwa ni Mungu katika kile kichaka. Kwa sababu, ile Sauti ilinena kutoka kichakani, ikimnukulia Maandiko, naye alishawishika ya kwamba Huyu alikuwa ni Mungu. Ndipo Mungu akasema, “Nitakuwa pamoja nawe.” Mnajua, hakuhusika kabisa na masumbuko ya Misri. Alikuwa amekuwa huko nje miaka arobaini, nao hao watumwa wakiwa mbali. Lakini wakati aliposhawishika kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kuwakomboa, alihusika mara moja kesho yake.

¹⁶³ Huyu hapa anashuka kwenda barabarani. Ungewazia ni tamasha la aina gani? Pamoja na Zipora akiwa ameketi juu ya nyumbu, mtoto Gershomu kwenye nyonga yake. Ndevu zinaning’inia chini namna *hii*, mwenye umri wa miaka themanini; kichwa chenyepara upara kiking’ara kwenye jua; fimbo iliyopinda mkononi mwake; akipaza sauti, “Haleluya!” Akishuka kwenda Misri, kuiteka. Naam.

Linaweza kukufanya utende kigeni.

¹⁶⁴ Huenda lilimfanya kutenda kigeni, bali alishawishika. Kwa nini? “Ninaenda pamoja nawe, Musa. Nitaichukua fimbo hii iliyo mkononi mwako, nami nitawakomboa watu Wangu.” Sasa, maskini fimbo ndogo iliyopinda haikuonekana kama ni kitu, lakini, ndugu, yeye alishawishika kwa sababu Neno la Mungu lilikuwa pamoja nayo.

¹⁶⁵ Ukijua Neno la Mungu liko pamoja nawe, na ndani yako, unaweza kushawishika.

¹⁶⁶ Wale wana wa Kiebrania, walishawishika ya kwamba Yeye alikuwa anaweza kutimiza Neno Lake, naam, mradi tu wangesimama juu ya Hilo. Mungu aliwaambia wasizisujudie sanamu. Hivyo ndivyo Mungu alivyomaanisha hasa. Nao walijua ya kwamba ikiwa hawakuinamia sanamu hiyo, kwamba Mungu

aliweza kulitimiza Neno Lake. Walishawishika kwamba Yeye aliweza. Ndipo waliposhawishika kuhusu kusimama pamoja na Neno Lake, Mungu alihusika kuhusu kusimama pamoja nao.

¹⁶⁷ Unaposhawishika kwamba Hili ni Neno la Mungu, Mungu anahusika kukushughulikia kwa Hilo. Umelijaribu, kote kwenye maeneo ya kigeni na kila mahali, wakati umeshawishika kwamba ni kweli. Lakini, huna budi kushawishika, kisha Mungu atahusika nawe. Lakini, kwanza, huna budi kushawishika kwamba ni Yeye, na Yeye hutimiza ahadi Yake, ndipo Mungu anahusika.

¹⁶⁸ Martha alishawishika kwamba kama Yesu akimwomba Mungu, ingetukia. Akasema, “Sijali yale hao wengine wasemayo. Sijali hata kama dada yangu Mariamu haliadini. Siamini, sijali yale rabi asemayo. Lakini, Bwana, kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Naye akasema . . . “Hata sasa, nimeshawishika, kama ukimwomba Mungu, Mungu atakupa. Litatukia. Ninashuka moja kwa moja, nikalibingirishe lile jiwe. Nitafanya maandalizi kwa ajili yake. Nimeshawishika.” Hakika.

¹⁶⁹ Ninamkubuka baba yangu, huko chini Kentucky, miaka kadhaa iliyopita. Mimea yote ilikuwa ikikauka. Ndipo yule mhubiri wa kale wa mzunguko akapitia kule, naye alikuwa mzee mzuri sana. Alipopiga magoti, yeye alikaa pale mpaka jambo fulani likatukia. Siku hiyo, wote walitaka kuomba mvua inyeshe. Baba akasema, wakati mzee huyo alipopiga magoti yake, naye akaiona hiyo mikono yenye makunyanzi imeinuliwa hewani, alisema, “Ee Mungu, nimekutumikia Wewe. Watu hawa ni Wako, nayo mimea yao inakauka.” Baba alisema alinyemelea akatoka nje ya hilo kanisa, akaenda huko nje akatoa matandiko kwenye nyumbu wake, akayatupa chini ya kanisa, maana alijua mvua ilikuwa inakuja. Kushawishika, naam, bwana, ndipo akahusika kuhusu matandiko yake. Ukiisha kushawishika!

¹⁷⁰ Martha alisema, “Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa. Hiyo ni kweli. Litatukia, kama ukimwomba Mungu.” Si hilo ni ajabu?

¹⁷¹ Yairo, akiwa na mfu nyumbani mwake, mtoto wake wa pekee, umri wa miaka kumi na miwili, msichana mdogo. Ujumbe ukaja, “Usimsumbue Bwana, kwa kuwa tayari amekufa.” Naye Yesu akasema . . .

¹⁷² Kwanza, yeye alimwambia Yesu, “Msichana wangu mdogo hata amekufa sasa, bali mimi nimeshawishika.” Haleluya! “Njoo, weka mikono Yako juu yake, atakuwa sawa.” Kushawishika!

¹⁷³ Alikuwa amesikia habari za Yesu. Alizijua kazi Zake. Alikuwa ni mwaminio wa siri. Chini moyoni mwake, yeye aliamini ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

Alishawishika kabisa ndivyo alivyokuwa. Mwajua, hilo si ni la kigeni? Mungu alimsukuma kwenye hiyo hoja.

¹⁷⁴ Mungu anajua jinsi ya kukusukuma. Kweli. Wakati mwingine Yeye hukupa maradhi, kila kitu kingine, apate kukusukuma tu kwake, uonyeshe rangi yako, kile ulicho.

¹⁷⁵ Akamsukuma. Yairo alisukumwa kuamini hilo. Kwa hiyo basi akaonyesha kile alichokuwa. Kasema, “Kama utakuja, uweke mikono Yako juu ya msichana wangu, ingawa amekufa, yeye ataishi.” Loo, jamani! Ninapenda hilo.

Nafikiri, Martha alisema jambo lile lile.

Yesu alishawishika Kwake, pia.

¹⁷⁶ Yule askari wa Kirumi, akida, alishawishika, kama tu angalimfanya Yesu kusema Neno. Msikilizeni askari yule, Mrumi, Mmataifa, kafiri. Alisema, “Mimi ni mtu chini ya mamlaka. Ninamwambia mtu *huyu*, askari *huyu*, ‘Wewe nenda *huku*,’ na anaenda. Kisha namwambia *huyu*, ‘Njoo,’ na anakuja.” Kwa nini? Alikuwa juu yake. Alikuwa akishuhudia nini? “Yesu, Wewe uko juu ya magonjwa yote. Uko juu ya yote. Kama ninaweza tu kukusikia Wewe ukisema Neno, mtumishi wangu ataishi. Nimeshawishika kabisa.”

Halafu basi, baada ya hayo yote, bado hatushawishiki. Mnaona?

¹⁷⁷ Ilikuwa ni kitu gani? Yesu alisema hiyo ilikuwa ni imani kuu. Hakupata hiyo katika Israeli. “Sema tu Neno.”

¹⁷⁸ Hili hapa, papa *Hapa*. “Mnapoomba, aminini kwamba mmepokea mliyoomba, nanyi mtapokea. Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka, wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako yale uliyosema.”

¹⁷⁹ Kisha kiri. Nini? “Kwa mapigo Yake mimi nimepona. Kwa neema Yake nimeokolewa. Kwa ahadi Yake nitatii, nami nitajazwa na Roho Mtakatifu.” Haya basi, kama umeshawishika ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake. Lakini kwanza huna budi kushawishika.

¹⁸⁰ Yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, alishawishika; haidhuru rabi alisema nini, na yale kuhani aliyosema, na yale mume wake aliyosema, na yale mtu mwingine yeyote aliyosema. Yeye alisema, “Huyo ni Mtu Mtakatifu. Yeye ni Mwana wa Mungu. Na kama ninaweza kuugusa upindo wa vazi Lake, hilo tu ndilo linalonipasa kufanya. Nimeshawishika nitapata afya.” Ingawa daktari anasema hawezi kupona, lakini yeye alisema, “Ninaweza kupona iwapo tu ninaweza kugusa upindo wa vazi Lake.” Alishawishika.

¹⁸¹ Yule mwanamke kisimani alishawishika ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, wakati alipokuwa ameiona ile ishara ya kimaandiko, kwamba alijua kile Masihi atakachokuwa. Kama nilivyosema asubuhi ya leo, yale maisha yaliyokusudiwa tangu

zamani yalikuwa yamekaa pale. Na punde tu yeye . . . Hilo, maji moto yaliyomwagwa . . . Maji baridi, hasa, yalimwagwa juu ya Neno hilo la uzima ambalo Mungu alikuwa amekusudia tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, yeye aliliona Hilo [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] upesi hivyo. Wakati, kulikuwako na wahudumu kule, hawakuliona Hilo; makuhani ambao hawakuliona Hilo; makuhani wakuu hawakuliona Hilo; makasisi wakuu hawakuliona Hilo; waliliita “ibilisi.” Naye maskini huyo kahaba, huko nje, Mungu alikuwa amekusudia hilo tangu zamani tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kama uliwahi kuwa kule, ulikusudiwa, pia.

¹⁸² Sasa, Biblia ilisema, “Katika siku za mwisho, mpinga Kristo atakuwa wa kidini sana, na kufanana sana na kitu kilicho halisi, hata ingewadanganya walio Wateule kama yamkini.” Lakini, haiwezekani. Hiyo ni kweli. Na, “Wote.” “Angewadanganya wote, walio juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo.” Tangu ule uamsho wa mwisho? Hilo halisikiki kama Biblia, sivyo? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] “Tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.” Hutawadanganya, maana wao wamekaa moja kwa moja katika Neno hilo. Wanapoyaona mambo hayo yakitokea, [Ndugu Branham anadata vidole vyake.] Ni Uzima, wanaushika sasa hivi.

¹⁸³ Wengine watatembea huku na huku, wakisema, “Aa, hakuna kitu katika Hilo. Huh!” Mnaona? Hawajashawishika. Hakuna kitu pale cha kuwashawishi. Hakuna kitu ndani yao, cha kuaminia.

¹⁸⁴ Mama alizoea kusema, “Unawezaje kupata damu kutoka kwa mboga nyekundu wakati hamna damu yoyote mle?” Kweli.

¹⁸⁵ “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.” Wanalijua Neno. Sauti Yake ni nini? Hii *hapa*. Kanuni hizi za imani hawazifuati. “Bali, wanaisikia Sauti Yangu, wanaifuata.”

¹⁸⁶ Mwanamke kisimani alishawishika kabisa. Kisha akahusika ya kwamba watu wake pia wangeiona ile ishara na kuiamini, akiisha kushawishika kwamba Huyu alikuwa ni Masihi. Kwa sababu, Yeye alimwambia mahali shida yake ilipokuwa. Akasema, “Bwana, tunajua ajapo Masihi, Yeye atafanya hilo.”

¹⁸⁷ Akasema, “Mimi Ndiye.” Alijua mtu ambaye angeweza kufanya jambo hilo hakika angekuwa akisema Kweli. Utukufu kwa Mungu! Naam, mtu ambaye Mungu angemtumia kwa njia hiyo asingesema uongo. Kweli. Atawaambieni Kweli. Kasema, “Mimi Ndiye.”

¹⁸⁸ Naye alichangamka sana wakati Nuru hiyo ilipopenya kupitia kwenye Neno hilo, akakimbia mjini. Alishawishika kabisa. Kama alipaswa kufanya hivyo, ama sivyo, yeye alikimbia mjini na kuwaambia hao marabi na makuhani, na wanaume wote mitaani, wanaume wa sokoni, na huko juu katika kila

duka. Basi akaenda huku na huku mtaani, akishuhudia, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Ichukue Biblia yako. Angalia kwenye magombo. Hiyo si ni Kweli, kwamba Huyu ndiye Masihi mwenyewe?” Alishawishika. Yeye atasimama kwenye ile hukumu na kuwahukumu maelfu ya watu kutoka Marekani huku. Hakika atawahukumu.

¹⁸⁹ Mwajua, Yesu alisema, “Malkia wa kusini atasimama katika ile hukumu, awahukumu, maana alikuja kusikia karama ya hekima, aliyokuwa nayo Sulemani, upambanuzi.” Ndipo kasema, “Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.” Hakika. Lakini hata hivyo watu wasingemwamini Yeye. Hakika.

¹⁹⁰ Alishawishika, naye aliwataka watu wake kushawishika. Mnaona? Akiisha kushawishika, basi alihusika kuhusu watu wake. Yeye alijua ya kwamba Huyu alikuwa ni Masihi. Alijua hivyo ndivyo Biblia ilivyosema lingetukia ajapo Masihi.

¹⁹¹ Akasema, “Tunajua kwamba Masihi, aitwaye Kristo, ajapo, Yeye atatwambia mambo hayo. Lakini hapana shaka Wewe ni nabii.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.”

¹⁹² Hapo alishawishika. Kwa sababu, alijua Maandiko yalisema hivyo, naye Huyu hapa. Alishawishika, kisha akahusika. Alienda akamwambia mtu mwingine.

¹⁹³ Sasa, Yesu alishawishika ya kwamba Yeye angefufuka katika siku ya tatu. Alishawishika sana, akasema, “Tharibuni hekalu Hili, nami nitalisimamisha siku ya tatu.”

¹⁹⁴ Kwa nini? Daudi, katika Maandiko, chini ya uvuvio, nabii. Daudi alikuwa ni nabii, mwajua. Daudi, chini ya uvuvio, alitabiri, na kusema, “Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.”

¹⁹⁵ Na Yeye alijua ya kwamba wakati fulani katika saa sabini na mbili, kabla uharibifu kuingia kwenye mwili huo, Yeye angefufuka. Saa sabini na mbili ni siku tatu mchana na usiku. Yeye alisema, “Liharibuni, nami nitalisimamisha tena,” alishawishika kabisa, hiyo ni kweli, kwamba angelisimamisha tena. Yeye alijua Maandiko hayawezi kushindwa. Haleluya!

¹⁹⁶ Nimeshawishika kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimeshawishika, katika hii huduma na huu Ujumbe, ninaohubiri, nimeshawishika kwamba ni Kweli. Nimeshawishika ya kwamba maono haya yanatoka kwa Mungu. Nimeshawishika tunaishi katika siku za mwisho. Nimeshawishika ya kwamba Roho yuyu huyu aliye juu yangu ni Roho Mtakatifu. Utukufu!

¹⁹⁷ Nimeshawishika kabisa. Nimeshawishika kwamba njia ya Roho Mtakatifu ni ya kweli. Nimeshawishika ya kwamba njia ya Biblia ni ya Kweli. Nimeshawishika ya kwamba Huyu ni Yesu Kristo hapa sasa. Nimeshawishika. Kama tukimwamini

dakika hii, nimeshawishika kwamba Yeye angeponya kila mtu mgonjwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Nimeshawishika Yeye angemwaga Roho Mtakatifu juu ya mahali hapa, mpaka kungekuwako na kelele kubwa mno, hata ingekuwa ni vigumu kujua yale yangetukia.

¹⁹⁸ Nimeshawishika. Ninaliamini kwa moyo wangu wote, sio kwa sababu mimi ni mzee. Nilihubiri hili nilipokuwa mtoto, asiyezidi umri wa miaka ishirini. Nimeshawishika tangu siku hiyo alipokutana nami mtoni. Haleluya! Nimeshawishika kwamba Yeye yupo hapa sasa. Nimeshawishika. Nayo Nguzo hiyo ya Moto ni Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa pamoja na Israeli nyikani, ndiyo Nguzo ile ile ya Moto iliyo pamoja na Kanisa siku hizi. Utukufu! Nimeshawishika ni kweli. Nimetoa maisha yangu kwa ajili Yake. Nimeondoka nyumbani na kila kitu, nikatoa yote niliyo nayo kwa ajili Yake. Nimeshawishika ni Kweli.

¹⁹⁹ Nimeshawishika Yeye yupo hapa sasa. Nimeshawishika kwamba Roho huyu aliye hapa sasa ni Roho Mtakatifu. Nimeshawishika kwamba tumebatizwa katika Roho Wake sasa hivi. Ninajua ni Kweli. Nimeshawishika kabisa kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimeshawishika, nimeshawishika kikamilifu.

²⁰⁰ Huyu Malaika alikutana nami huko juu na kuniambia yale aliyofanya. Nilisimama mbele ya makafiri kwa maelfu, na makumi elfu. Mnasema, “Hivi huogopi?” La, bwana. Nimeshawishika ya kwamba inatoka kwa Mungu. Nimeshawishika kwa sababu ilikuwa ni ya Kimaandiko. Nimeshawishika ya kwamba ni Malaika wa Bwana. Ninaamini hilo kwa yote yaliyo ndani ya moyo wangu. Amina. Nimeshawishika, kama tungemwomba Mungu chochote, Yeye angetupatia. Mnaogopa tu. Msiogope. Yeye yupo hapa.

²⁰¹ Nimeshawishika ya kwamba Roho yuyo huyo mnayemhisi, Roho Mtakatifu anayetenda kazi ndani yetu, nimeshawishika kwamba Huyu ni Kristo. Amina. Nimeshawishika kwamba sasa hivi, kwamba, Hii ndiyo ninayoitazama, duara hii ya Nuru mbele yangu, nimeshawishika kwamba huyo ni Roho Mtakatifu. Nimeshawishika ono hilo liko juu ya macho yangu. Ninajua Yeye yupo. Amina. Ninampa changamoto kila ibilisi ulimwenguni, saa hii. Kweli! Yeye ni Mungu. Kristo si nabii tu, Yeye ni Mungu, si chochote pungufu yake.

²⁰² Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Kamwe siwezi kuhubiri zaidi. Hum! Upako wa jinsi gani! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁰³ Jina la Bwana libarikiwe! Nimeshawishika kabisa ya kwamba Yeye ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele!

²⁰⁴ Baba wa Mbinguni, nimeshawishika ni Wewe. Ninaomba, Mungu, kwamba ninapoondoka kwenye jukwaa hili, usiku wa leo, kwamba Wewe utafanya jambo fulani maalum.

Wathibitishie hawa watu, mara nyingine tena, kwamba ni Wewe. Ninalikabidhi kusanyiko hili Kwako. Bwana, tuko mikononi Mwako. Fanya nasi upendavyo. Katika Jina la Yesu. Amina.

Jambo fulani lilitukia. Nimeshawishika kwamba Mungu yupo hapa.

²⁰⁵ Alisambaza kadi za maombi, kadi zozote za maombi? [Mtu fulani anasema, “La.”—Mh.] La. Hatuzihitaji. Nimeshawishika kwamba Yeye yupo hapa. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Ndiyo.”]

²⁰⁶ Kama umeshawishika kwelikweli, sema, “Yesu, ninakugusa Wewe, kwa mambo ya udhaifu wangu. Ninaamini ya kwamba Ndugu Branham amesema Kweli. Yeye ni mwanadamu tu. Wewe ni Mungu. Lakini ninaamini yeye alisema Kweli, maana ni Neno. Jalia litendeke, Bwana. Jalia yeye aseme nami na kuniambia. Anifanye nishawishike.”

²⁰⁷ Hii hapa, tayari mkutanoni. Yule mama anayeketi pale, yeye anaombea tatizo la wasiwasi. Msichana wake mdogo, pamoja naye, amedumaa. Mtaamini jambo hilo? Mama mgonjwa nyumbani. Kuwa na imani. Usitie shaka. Unaweza kupata uliyoomba.

²⁰⁸ Nimeshawishika ya kwamba Malaika yule yule aliyeshuka katika mfano wa Mwanadamu na kuzungumza na Ibrahimu, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Ndiye yule yule hapa usiku wa leo. Aliahidi ingekuwa. Ninaamini ya kwamba Malaika yuyo huyo anatutia mafuta, kwa sababu alikuwa ni Mungu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, Sara, mahali fulani hapa ndani, wewe nena na Mungu. Nimeshawishika, dada. Nimeshawishika ndugu, ninajua ni Kweli. Hakika ni kweli.

²⁰⁹ Yupo mama anayeketi nyuma yangu. Yeye yuna ugonjwa wa moyo. Ameketi moja kwa moja nyuma yangu. Simjui. Amesimama mbele yangu. Ni mwanamke mwenye umri wa makamu. Hatoki hapa. Ametoka Virginia. Bibi Fox, Yesu Kristo anakuponya. Ameketi mumu humu ndani. Hebu tuone. Ndiye huyu, papa *hapa*. Amini.

²¹⁰ Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

²¹¹ Unawazia nini juu yake, mama? Mimi na wewe hatufahamiani, mmoja na mwingine? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini? Una tatizo la kichwa. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bibi Moore. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Nenda nyumbani. Uponywe.

Mnaamini?

²¹² Sasa mtu fulani hapa juu, mbele zangu hapa. Hii hapa, mtu fulani. Ni mwanamke. Yuna kansa kwenye titi. Bibi Rhodes, mwamini Bwana Yesu Kristo. Simjui mwanamke huyo. Mungu

anamjua. “Waweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Kweli.

²¹³ Mwanamume anayeketi huko, akiomba, kutoka Tulsa. Bw. Harwood, mwamini Bwana Yesu Kristo. Nenda, ukaponywe. Uwe na imani. Hiyo tu ndiyo uliyo nayo. Simjui mtu huyu, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hatufahamiani. Lakini hilo ni kweli. Kwa nini? Aligusa kitu Fulani.

²¹⁴ Mmeshawishika? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mmeshawishika ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake? [“Amina.”] Kama mmeshawishika, ni wangapi wenu walio na haja?

²¹⁵ Sasa, hakika, kama vile yule mwanamke alivyowazia kisimani... Waulizeni watu hawa. Nendeni, kazungumze nao, popote wao...

²¹⁶ Ninamwona mwingine. Naam, mwingine. Sikilizeni, angalieni kama ni kweli ama si kweli. Sasa inalizunguka hili jengo. Jengo lote limetiwa mafuta, mahali pote. Nimeshawishika ya kwamba Uwepo wa Yesu Kristo utamponya kila mtu hapa.

²¹⁷ Mmeshawishika vile vile? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mmeshawishika ninawaambia Kweli? [“Amina.”] Mungu anathibitisha ninawaambia Kweli. Basi, ninaamuru kwamba msimame kwa miguu yenu na kuukubali uponyaji wenu, katika Jina la Yesu Kristo. Kama mmeshawishika, mwinulieni mikono yenu, na mumppe Yeye sifa.

²¹⁸ Baba wa Mbinguni, Roho Mtakatifu, lijaze jengo hili. Wameshawishika kwamba Shetani ameshindwa.

²¹⁹ Katika Jina la Yesu Kristo, Shetani, toka mahali hapa. Tumeshawishika kwamba huu ni Uwepo wa Yesu Kristo hapa. Nalo litatimizwa. Amina.



KUSHAWISHIKA KISHA KUHUSIKA SWA62-0610E

(Convinced Then Concerned)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 10 Juni, 1962, katika Shule ya sekondari ya Juu ya Aberdeen huko Aberdeen, Carolina ya Kaskazini, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org